# Usawiri wa Wanawake wenye Uwezo katika Muziki wa Bongo Fleva nchini Tanzania

*Zawadi Daniel Limbe*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Kwa kutumia mkabala wa ulinganishi, makala haya yanajadili uhusiano wa kijinsia unaobainishwa katika muktadha ambao mwanamke ndiye mmiliki wa mali na ambaye ana fursa katika vyombo vya kufanya maamuzi. Tafiti nyingi zinazungumzia suala la ujinsia zikijikita katika kumwangalia mwanamke kama chombo kinachotumiwa na wanaume katika kutimiza matakwa yao. Pia, zinasawiri namna mwanamke anavyozingirwa na mfumo usio mpa fursa za uhuru binafsi pamoja na maendeleo. Makala haya yanalenga kuleta ukengeushi wa suala hili, kwa kumtazama mwanamke ambaye ana uwezo wa kimaendeleo, mathalani uwezo wa kielimu, kiuchumi, kisiasa, na hata kushiriki katika vyombo vya maamuzi, jinsi ambavyo uhusiano wake ndani ya jamii unavyosawiriwa. Kwa kutumia nyimbo za muziki wa bongo fleva, kama fasihi simulizi pendwa nchini Tanzania, makala yatajadili mahusiano yake na jinsia nyingine na hata na jamii kwa ujumla. Katika makala haya, ulinganishi wa nyimbo za mziki wa bongo fleva zilizoimbwa na jinsia tofauti utafanyika.**

**Maneno Muhimu:** *Mkabala wa Ulinganishi, Kizazi Kipya, Bongo Fleva, Uhusiano wa Kijinsia*

## Utangulizi

Tahakiki nyingi zinazozungumzia muziki wa Bongo fleva (ambao wachambuzi wengine wanauita muziki wa *kizazi kipya* au *Hip hop)* zinataja asili yake kuwa ni Marekani hasa kutoka kwa Wamarekani Weusi. Inaelezwa kuwa chimbuko la muziki huu ni kutoka katika nchi za Magharibi hasa Marekani, ambapo Waafrika waliopelekwa huko kama watumwa waliibua aina hii ya muziki ili kuelezea madhila waliyokuwa wakikabiliana nayo vilevile waliutumia kama njia ya kujiliwaza. Katika kufafanua chimbuko hili Omari (2006:73) anasema:

> “Hip hop ilianzishwa na Wamarekani weusi huko The Bronx, New York Marekani mnamo miaka ya 1970. Wamarekani weusi wana asili ya Afrika, ambao babu zao walichukuliwa kwenda Marekani kama watumwa…mizizi hasa ya muziki wa rap ni Afrika, kwani mbali na kuanzishwa na Wamarekani weusi, muziki wa rap una sifa mbalimbali za kimuziki na za kifasihi simulizi za Kiafrika, kwani pamoja na matumizi ya midundo au ridhimu, usimulizi, kiitikio na majigambo.”

Huu umekuwa ni mziki maarufu sana nchini Tanzania, ukiimbwa na kusikilizwa na karibu makundi rika yote, yaani watoto, vijana, wanawake na hata watu wa makamo (wazee). Pamoja na kwamba muziki huu ulikumbana na changamoto ya kutokukubaliwa na baadhi ya makundi ndani ya jamii nchini Tanzania, hasa wazee na watu wenye rika la utu uzima kama anavyobainisha Mahenge (2010), hata hivyo yapo mabadiliko makubwa kuhusu kupokelewa kwa nyimbo za muziki huu hivi sasa, kutokana umaarufu ambao muziki huu umejizolea. Shutuma kuwa muziki huu unahusisha uhuni kutokana na aina ya mavazi yanayovaliwa na waimbaji wake, pamoja na dai kuwa dhamira (maudhui ya muziki huu ni mapenzi na masuala ya kingono tu, mambo haya yanaonekana kupoteza nguvu kwani kupitia muziki huu masuala mengi na muhimu ya kijamii, katika nyanja zote za kimaisha yanaelezwa kupitia nyimbo mbalimbali. Mathalani, kupitia muziki huu masuala mengi na muhimu ya kijamii, kisiasa, kitamaduni na hata kiuchumi yanabainishwa kwa upana wake na wasanii wa Bongo fleva (Omari, 2006, 2008; Bulaya, 2010; Mnenuka, 2010; na Samwel, 2010). Katika makala haya, tunaweza kusema kuwa Bongo fleva ni muziki ambao unaimulika jamii katika nyanja zote za

kimaisha. Nafasi ya mwanamke ni miongoni mwa mambo ambayo yanajitokeza sana katika muziki huu. Kutokana na ujitokezaji huu, ndiyo maana makala haya yanadhamiria kuchunguza namna mwanamke ambaye ana uwezo na nguvu za kiuchumi, au kisiasa, ama hata kielimu n.k. anavyosawiriwa katika muziki huu. Usawiri huu ni pamoja na jinsi uhusiano wake na jamii unavyojitokeza

Katika tamaduni nyingi, kiuchumi wanawake wameonekana kuwategemea zaidi wanaume (hasa baba zao, kaka, mme na watoto wao wa kiume) kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Vilevile, mila na desturi nyingi duniani zenye nguvu zinamnyima fursa mwanamke kujikwamua kiuchumi (Schipper, 2006). Wanawake wanachukuliwa kuwa watu wa jikoni ambapo katika jamii, majukumu yao makubwa ni kufanya kazi zinazohusiana na utunzaji nyumba na familia. Kazi hizi ni kama kupika na kuandaa chakula, kufanya usafi wa nyumba, kulea na kutunza watoto pamoja na kazi ndogondogo za mikono, n.k. Katika kuelezea hali hii, Schipper (2006:214) anazitaja kazi hizi na kuziweka katika kile anachokiita yeye kuwa ni **C** nne ambapo anasema:

> "Childcare (from nursing to rocking and all other forms of care)
>
> Cleaning (including sweeping, washing etc)
>
> Cookery (including all the preparation from fetching water, collecting firewood, gathering herbs and other ingredients, to grinding, cooking, baking and so forth)
>
> Craft (spinning, weaving, needlework, knitting, etc)"

Aidha, wanawake wamekuwa wakifungamanishwa na vitu vingi kama vile, mimea, wanyama, matukio ya asili kama mvua, radi, mahali kama jikoni, chumbani na sehemu kama vile mbingu, dunia, pepo, maji, n.k. (Momanyi, 2001 na Schipper (2006). Mwanamke (hasa mwenye ujuzi) pia, amehusishwa na shetani. Mathalani zipo methali mbalimbali ulimwenguni zinazomlinganisha mwanamke na shetani. Akifafanua hili Schipper (2006:248) anasema:

> "In Western proverbs knowing is often associated with the Devil. When women build a house for example, not even the Devil can destroy it, and as it is said in Polish: The Devil swallowed a woman, but he could not digest her."

Katika fasihi simulizi pendwa ya Kiswahili, wahakiki wengi ambao wamechunguza bongo fleva na jinsia wanaonekana kuegemea katika mtazamo wa kumwangalia mwanamke masikini na tegemezi. Wengi wanaeleza namna mwanamke anavyosawiriwa katika nyimbo hizi na matokeo ya jumla ya wahakiki hawa yanabainisha kuwa, katika nyimbo za bongo fleva mwanamke anaonekana kuwa ni kiumbe dhaifu/duni na tegemezi, pia anatumiwa kama chombo ambacho kinatumiwa na wanaume katika kujistarehesha kingono. Kwa mfano, Mnenuka (2010) amechunguza taswira ya mwanamke katika muziki wa bongo fleva ambapo aliangalia namna udhaifu wa mwanamke unavyobainishwa kupitia majina/maneno kama vile, samaki, bata, ndege, vocha n.k. Hitimisho lake linadhihirisha kuwa mwanamke katika muziki wa bongo fleva anasawiriwa kama malaya na kiumbe anayetumiwa na wanaume kukidhi matakwa ya kingono.

Vivyo hivyo, Jilala (2010) naye anatoa hitimisho linaloonesha kuwa mwanamke ni kiumbe duni dhaifu na tegemezi, pale alipokuwa akichunguza sitiari mbalimbali zinazotumiwa katika nyimbo za bongo fleva jinsi zinavyomzungumzia mwanamke**.**

Hata hivyo, tukitazama kwa undani kuhusu uchunguzi wao, wahakiki hawa wanajikita zaidi katika kumwangalia mwanamke ambaye ni tegemezi na asiye na uwezo, makala haya yanalenga kuangazia upande mwingine wa mwonekano wa mwanamke. Makala haya yanachunguza katika muktadha ambao mwanamke si tegemezi tena mathalani ana mali (pesa), au ni kiongozi, ama ana elimu n.k. mwanamke huyu kupitia nyimbo za bongo fleva anasawiriwaje? Mahusiano yake ndani ya jamii yanaelezwaje? Tunatumia nyimbo za bongo fleva kama kiwakilishi cha mtazamo wa jamii kwani fasihi ni kioo cha jamii.

Suala la uwezo wa mwanamke limejadiliwa pia katika kazi nyingine za fasihi. Mathalani Schipper (2006:207) anaeleza juu ya jambo hili alipokuwa akichambua usawiri wa mwanamke katika methali za jamii mbalimbali duniani. Anasema:

> "Proverbs talk about female power in a variety of ways. From denying its very existence to openly expressing the fear of its destructive effects. The principal rule for women is never to reveal that they do have power, knowledge and other extraordinary mental or artistic abilities. A wife in partcular should not exhibit her talents and qualities (except in the domain of housekeeping and child care), and she would certainly refrain from openly having the upper hand over her husband, unless she wants to ridicule him in public, thus provoking his anger and consequently, risking violence or divorce."

Kwa mujibu wa Schipper (keshatajwa), kinachoonekana katika methali, uwezo wa mwanamke haupaswi kujidhihirisha hadharani au hata haupaswi kuwa juu ya ule wa mwanamume. Mwanamke anapaswa kuonesha ujuzi na ufahamu wake katika masuala yahusuyo shughuli za ndani ya nyumba yake tu si zaidi ya hapo. Kufanya hivyo kutazidi kulinda heshima yake ili asionekane tishio kwa mmewe. Tunachoweza kusema hapa ni kwamba, utamaduni wa jamii unamtaka mwanamke kushuka na kuonekana mtu wa hali ya chini ama kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume hata kama mwanamke huyu ana ujuzi, elimu, au uwezo kuliko mwanamume. Kwa hakika mtazamo huu unalandana sana na matokeo yaliyotolewa na Mnenuka (2010) na pia Jilala(2010) hapo juu, kwani katika mahitimisho yao wanaonesha kuwa, katika nyimbo za bongo fleva mwanamume ndiye mwenye uwezo na nguvu za kiuchumi na kijamii kwa ujumla, na hivyo hutumia nafasi yake hiyo kumtawala mwanamke kwa jinsi anavyopenda. Hata hivyo, lengo la makala haya ni kuona katika muktadha ambao mwanamke hayuko katika hali hiyo kiuchumi (utegemezi) anaelezwaje katika nyimbo za bongo fleva. Uhusiano wake na jamii iliyomzunguka (hususan mmewe) unabainishwaje.

**Usawiri wa Mwanamke Mwenye Nguvu/Uwezo katika Bongo Fleva**

Katika uchambuzi wetu tutatumia jumla ya nyimbo tano za bongo fleva kutoka kwa wasanii mbalimbali. Nyimbo hizi ni, *Narudi Kijijini* wa Best Naso, *Mtoto wa Geti Kali* wa Inspekta Haroun, *Mademu Watafutaji* wa AY na Stan Boy, *Zali la Mentali* wa Prof J na *Wanaume kama Mabinti* wa Lady Jaydee. Aidha pale panapohitajika nyimbo nyingine zitarejelewa.

**Mahusiano ya Kindoa na Mapenzi**

Katika wimbo wa *Narudi kijijini* wa Best Naso, mwanamke anasawiriwa kuwa ni mbabe na asiye mthamini na kumjali mmewe (anampuuza, hamheshimu). Msanii analalamika kuwa hali hii inasababishwa na kitendo cha mkewe kumtoa kijijini na kisha kumweka ndani (kumuoa). Anamlaumu mkewe kwa kusahau kuwa yeye alimkubali kwa sababu ya kumpenda si kwa sababu ya pesa zake.

Hata hivyo, kuna ukiushi wa utamaduni hapa kwani katika utamaduni wa Kiafrika (hususani Afrika Mashariki, Tanzania ikiwamo) mwanamume ndiye huoa. Kuoa ni kutenda na kuolewa ni kutendwa. Pengine dhana hizi hazijatokea kwa nasibu tu kwani zinabeba maana ya kimamlaka ndani yake. Anayeoa ndiye huwa kiongozi mwenye mamlaka na ni kichwa cha familia. Muoaji ndiyo hutoa mahari kwa familia ya muolewaji. Hali hii humpa uwezo na mamlaka ya kuwa kichwa cha familia. Kulingana na utamaduni wa Kiafrika, mwanaume ndiye kichwa cha familia na yeye ndiye huoa. Katika wimbo wa *Narudi kijijini* mwanamume analalamika kuwa mkewe anamnyanyasa kwa sababu yeye (mke) ndiye amemuoa mwanamume. Msanii anasema.

> "Eti kisa niko nyumbani kwako umenioa"

Ingawa katika wimbo huu hali hii inaelezwa kutokea, hata hivyo jambo hili si la kawaida sana katika utamaduni wa Kiafrika, kwa mwanamke kumuoa mwanamume. Kinachoonekana hapa ni kuwa mwanamke mwenye pesa na uwezo wa kiuchumi anaweza kuoa na hivyo kuwa kichwa cha familia jambo linalopindua na kukiuka kabisa mila na desturi zilizozoeleka katika jamii yetu. Ingawa hali hii pia inatuashiria kwamba pengine uwezo wa mwanamume kuoa na kuwa kichwa cha familia umejengwa na misingi ya fedha na mali, hivyo, kama mwanaume atakosa vitu hivi anaweza kupoteza uwezo huu. Si kwamba ukiwa mwanamume unapata, uwezo na mamlaka ndani ya familia na jamii

kwa ujumla, kwani hata mwanamke anaweza kupata haya kama naye ana nguvu ya kifedha. Kutokana na hili, ni dhahiri kuwa mwanamke mwenye pesa ndani ya jamii anaonekana kufanya mambo ambayo kwa kawaida ndani ya jamii hufanywa na wanaume. Hata hivyo, baada ya kupata haya mwanamke anaonekana kuwa mbabe kwa mmewe. Kupitia wimbo huu ambao unamuonesha mwanamke ambaye ana uwezo na mamlaka ya kutawala familia analalamikiwa kutumia ubabe na kutomthamini mmewe. Inawezekana ni kutokana na mtazamo huu jamii inasita kuwapa wanawake uwezo na mamlaka kwani kwa kufanya hivyo, kutapindua mazoea pamoja na utamaduni uliopo na vilevile wanawake pindi wanapopata uwezo kimaisha hubadilika kwa kuwageuka waume zao kwa kuwaona hawana thamani tena mbele yao. Katika wimbo huu, mme analalamika kupuuzwa na mkewe kutokana na ukweli kuwa mkewe anaweza kuondoka nyumbani kwa zaidi hata ya siku tatu bila kuaga ama kutoa taarifa kwa mmewe. Schipper (2006) anaeleza pia kuwa katika miongo ya nyuma wanawake katika jamii za Ulaya hawakupata fursa ya kielimu kwa hofu ya wanawake hao kugeuka miungu watu na wakiuka maadili.

Uhusiano wa kindoa wa mwanamke dhidi ya mme wake katika wimbo huu unamuonesha mwanamke kama mtu mwenye sauti, mamlaka n.k. Hali hii ni tofauti na wanawake tegemezi kama ambavyo Omari (2008) anawaelezea kuwa katika uchambuzi wake wa nyimbo za watoto, mwanamke anaonekana kuwa hana sauti wala mamlaka na hayuko huru kwani haruhusiwi hata kutoka nje ya nyumba bila ruhusa ya mmewe, pia hata kutumia baadhi ya vitu vya ndani pasipo idhini kutoka kwa mmewe. Katika wimbo huu wa *Narudi Kijijini* mme analalamikia vitendo vya mke wake kuamua kurudi usiku, au kutokurudi kabisa nyumbani, au hata kurudi nyumbani akiwa amelewa n.k. Katika familia za Kiafrika, si kawaida sana kusikia mme akilalamikia mambo kama haya. Haya hufanywa sana na wanaume ambao ndiyo huheshimika kuwa viongozi wa familia. Hata hivyo, mambo haya yanachukuliwa kuwa mambo ya kawaida kufanywa na wanaume lakini ni ajabu kufanywa na mwanamke. Na mwanamke afanyaye haya huonekana mpotofu wa maadili na anayekiuka utamaduni.

**Unyanyasaji na Ukatili**

Katika muziki huu wa bongo fleva, mwanamke anasawiriwa kuwa kiumbe katili na mnyanyasaji. Anaonea na kunyanyasa watu walio chini yake ama ambao ni masikini. Katika wimbo wa *Narudi Kijijini*, mke anaamua kumfukuza mama mkwe wake kwa sababu hakumpenda tu. Kwa hakika kitendo hiki ni ajabu sana kwani kazi nyingi za fasihi hususani nyimbo zinapoelezea uhusiano wa mama mkwe na mke wa mwanawe motifu iliyozoeleka ni ile ya mama mkwe kumnyanyasa mkwewe. Kitendo cha mama mkwe kufukuzwa nyumbani kwa mwanawe wa kiume kinatufanya tufikiri kuwa pengine utegemezi wa kijana wake kwa mkewe ndiyo chanzo cha wote wawili kunyanyasika. Vilevile, mke anaondoka na kumuacha mme wake nyumbani yeye anarudi usiku au wakati mwingine harudi kabisa nyumbani. Analalamikiwa pia kuwa wakati mwingine hurudi nyumbani akiwa amelewa na kumtukana matusi mmewe. Hali inayotuonesha kuwa mwanamume ananyanyaswa na mkewe. Msanii anasema

> "Kila urudipo nyumbani
>
> Umelewa, unanipa matusi
>
> Maama.... leo una siku ya tatu hapa nyumbani hujalala na kuuliza unanitusi maamaa!"

Katika wimbo huu, mme analalamika kuwa mkewe anamnyanyasa, anamfanya kama ni mtumwa na hata mahusiano yao yametawaliwa na ubabe wa mkewe. Kutokana na manyanyaso ambayo mme anayapata kutoka kwa mkewe, maisha yao si ya maelewano. Wahakiki wengi ambao wameshughulikia mahusiano ya kijinsia katika kazi za fasihi wanaelezea suala la ukatili kama jambo ambalo linawapata sana wanawake kwa kufanyiwa na waume zao. Kwa kiasi kikubwa hawataji ukatili unaowapata wanaume, wao wameegemea zaidi kwa kumwangalia mwanamume kama kiumbe katili na mnyanyasaji. Hata hivyo, katika mashairi haya ya bongo fleva tunaona mwanamke naye anatajwa kama kiumbe mnyanyasaji na katili dhidi ya watu walio chini yake hususan pale anapokuwa na nguvu na mamlaka ndani ya jamii.

**Dharau na Kutokujali**

Katika nyimbo za bongo fleva zinazomzungumzia mwanamke mwenye uwezo, na nguvu za kiuchumi, mwanamke anasawiriwa kuwa mwenye dharau na asiye na heshima, utu na mwenye kujisikia. Haya yanajitokeza katika nyimbo kama vile za *Zali la Mentali*, *Mtoto wa Geti Kali,* na *Narudi Kijijini* ambapo zote zinabainisha vyema hali hii. Katika *Zali la Mentali*, msanii anasimulia juu ya mwanamume masikini kuvutiwa kimapenzi na binti ambaye kihaiba anaonekana kuwa mwenye uwezo, hata hivyo, binti huyu anamkataa kwa njia ya dharau. Anamkataa kwa kumtukana na kumkejeli kwa vile yeye ni masikini. "Masikini koma hii ni ngoma ya ghali "

Wimbo wa Inspekta Haroun wa *Mtoto wa Geti Kali* unaonesha pia kuwa wanawake wenye uwezo hawawezi au sio rahisi kuwa na mahusiano mazuri na wanaume wanaowazidi kipato. Msanii anasema amempenda msichana lakini anajua hawezi kumkubali kutokana na tofauti za kiuchumi. Mwanamke anatoka katika familia ya kitajiri na yeye ni masikini hivyo hawawezi kuishi pamoja.

Japokuwa hali hii kinyume chake sio ajabu hata kidogo. Nyimbo nyingi zinasimulia juu ya wanawake masikini kutaka kuwa na waume/wapenzi wenye uwezo ama fedha ili waweze kuwatumia kama daraja la kuwainua kimaisha. Nyimbo kama vile *Valuvalu* wa Chameleon zinazungumzia hali hii. Katika nyimbo hizi ama wasanii wanalalamika kuwa wapenzi wao hawakuwapenda kwa dhati bali walifuata pesa tu au wanawataka wapenzi wao kutulia wasitafute au kulaghaiwa na wanaume wengine wenye pesa na uwezo zaidi.

Katika *Narudi Kijijini* pia msanii anasema pesa ndiyo inamfanya mkewe ajisikie na ajenge dharau kwake kwa sababu yeye hana pesa kama mkewe.

> "Najua pesa inakufanya ujisikie na unaweza kumnunua umtakaye"...

Hivyo, mtazamo huu unaonesha kuwa mwanamke anapopata pesa au madaraka na kuwa na nguvu katika maamuzi huwa jeuri, mwenye dharau na ambaye anakosa heshima kwa mumewe na penginie hata kwa jamii tukimrejelea mama mkwe katika *Narudi kijijini*. Hata hivyo suala hili ni la mjadala kwani inawezekana kuwa matendo hayo yanaweza kufanywa na mwanamke sio kwa sababu ya fedha au nguvu alizonazo bali kwa sababu ya hulka yake tu. Kwani katika wimbo wa *Zali la Mentali* msanii anafanikiwa kuonesha upande mwingine wa mwanamke huyu pale anapokutana na binti mwenye uwezo lakini wanapendana na kuoana kisha wanaishi vyema kwa maelewano mazuri ndani ya nyumba.

> "tuliishi.............
>
> Kila siku ikawa ni kama sherehe" ...............

Hivyo, inawezekana kuwa mtazamo wa mke kuwa mwenye dharau unatokana tu na hofu waliyonayo wanaume juu ya kumwezesha mwanamume. Hofu hii inaweza kuwa imetokana na mfumo wa jamii wa kumjenga mwanamume kuwa mwenye nguvu na kuzuia uwezo wa mwanamke kujitokeza kwa kuzidi ule wa mmewe (rejea Schipper 2006:214).

**Kutumia Fedha Kufanya Uovu**

Mwanamke katika nyimbo hizi za bongo fleva anaelezwa kutumia pesa zake kama njia ya kufanya mambo yasiyofaa/pendeza ndani ya jamii. Kwa mfano kutumia pesa zake kuwapata kimapenzi vijana wadogo ambao kiumri ni sawa na watoto wake. Maneno kama *"Sugar mamii*".... yanaashiria hali hii. Mathalani katika wimbo wa Lady Jaydee *Wanaume kama Mabinti* mwimbaji anasema: "Hupenda kuwaliwaza wamama watu wazima."

Kauli hii inaeleza juu ya mahusiano ya wanawake watu wazima (wenye umri mkubwa) dhidi ya vijana wadogo ambao ni sawa na watoto wao. Pengine jambo hili linaonekana kukiuka maadili ya Kiafrika, kwani kulingana na utamaduni wa Kiafrika si vyema kijana wa kiume kuwa na mahusiano na mwanamke ambaye kiumri ni sawa na mama yake mzazi.

Katika kazi za fasihi, wanaume wenye pesa wanatajwa kutumia pesa zao kuwalaghai wasichana wadogo kwa lengo la kufanya nao mapenzi. Kwa mfano Swaleh (1997:28) anabainisha hili katika uchambuzi wake wa riwaya ya *Tata za Asumini*, anasema:

> "Mkejel is an old tycoon who entices young women into his arms by
> the allure of money and the power that goes with it."

Vilevile, wanaume wenye pesa huwa ni kimbilio la wanawake katika kuepuka kuishi maisha magumu, mathalani katika *Tata za Asumini*, Miriam anaamua kuolewa na mzee Mkejel si kwa sababu ya upendo kwake bali kwa sababu za kiuchumi tu (Swaleh, 1997). Vivyo hivyo, wanawake nao katika bongo fleva wanaelezwa kufanya tabia kama hiyo kwa vijana wa kiume.

Kwa ujumla, mtazamo hasi kuhusu wanawake wenye elimu na uwezo kimaisha unaojitokeza katika nyimbo za bongo fleva, unaelezwa pia na Schipper (2006) wakati akichambua jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika methali mbalimbali ulimwenguni. Anaeleza kuwa katika bara la Ulaya hapo zamani (kabla ya karne ya 20), wanawake walionekana kubaguliwa katika kupata elimu na ujuzi mbalimbali kutokana na hofu ya jamii kuwa watafanya mambo yasiyofaa ndani ya jamii. Anaeleza kuwapo kwa methali maarufu iliyosema "*A woman who knows Latin will never find a husband"* ( Latin ilichukuliwa kuwa ni elimu pamoja na ujuzi/ maarifa.) iliaminika kuwa wanawake wakipata elimu sawa na wanaume watabadlika na kuwa viumbe/ watu wasio na heshima, utii na wavunja maadili. Schipper (keshatajwa) anaendelea kufafanua kuwa ni hadi karne ya 20 bado baadhi ya sehemu huko Ulaya, wazazi hawakupendelea mabinti zao kwenda vyuo vikuu kutokana na hofu ya watoto wao kubadilika kitabia endapo watapata elimu. Vilevile, Balisidya (1982) anasema:

> "The Tanzanian woman will be considered with respect to her identification as an object without any social and economic status as human being, in other words, without liberty, treated merely as mans subordinate, servant or slave. In this capacity a woman's role is that of being owned as property in the form of a commercial item or as a tool for economic production."

Anachoeleza hapa ni kuwa, mwanamke ataheshimika na kutambulika kama kiumbe ambaye anamilikiwa na mmewe si kwa sababu ya hadhi ya kiuchumi na kijamii.

**Ni Kielelezo kwa Jamii**

Katika baadhi ya nyimbo za bongo fleva pia, mwanamke anasawiriwa kuwa ni kielelezo na fahari kwa jamii yake. Ni mtu ambaye anastahili kuigwa na jamii. Mathalani katika wimbo wa *Mademu Watafutaji* wa A.Y & Stan Boy wanamuelezea mwanamke kuwa kielelezo cha kuigwa na anayekubalika katika jamii.

Msanii anasema:

> "Nimemvulia kofia watu wamemsifia kwani amezidi
>
> Uwezo nzuri nazo tabia, hacheki cheki hovyo
>
> Anachenji si kidogo ni shosti tena wa kibongo anastahili kuchekisheki
>
> Bingo bonge la modo na mvuta bingo sometime tena mpango
>
> Haendekezi mapenzi…"

Kauli za "nimemvulia kofia" na "bonge la modo" zinabainisha sifa ambazo msanii anampongeza mwanamke wa aina hii. Hivyo, anaona kuwa tabia hizi zinafaa kuigwa na wanajamii wote hasa wanawake. Aidha, anawahimiza wanawake wengine/ambao yeye anawarejelea kuwa wanaolala, waige mfano huu ili kuepuka kuishi maisha ya kudhalilishwa na kuishi katika mfumo ambao mwanamke ni tegemezi (msanii ametumia neno golikipa kurejelea utegemezi wa mwanamke).

**Mwenye Msimamo**

Nyimbo nyingi zinamrejelea mwanamke kama kiumbe asiye na msimamo na mwenye kutumiwa na mwanamume kama chombo cha starehe. Omar (2008) anataja baadhi ya sifa zisizofaa za mwanamke ambazo zinaelezwa sana katika muziki wa bongo fleva kuwa wanawake ni watu wasio na uaminifu, watu wenye uwezo mdogo kiakili wazinzi na malaya. Vilevile, Momanyi (2001:59) anaeleza:

> "Mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert anaonekana kuwa kiumbe asiyeaminika. Anasema itikadi ya kiumeni iliyojipenyeza kwenye dini na kuenea katika utamaduni wa Kiislamu ilimchukua mwanamke kama kiumbe hatari aliyepaswa kutengwa na wanaume ili asiwaingize katika dhambi."

Kauli hii ni dhahiri kuwa inawaonesha wanawake kuwa ni viumbe wasio na msimamo na wasioaminika. Mnenuka (2010) naye anaungana na mtazamo huu katika mahitimisho yake, pale alipokuwa anachunguza taswira ya mwanamke katika muziki huu akiegemea nyimbo za mduara. Jilala (2010) naye anabainisha mwendelezo wa sifa hizi, pale anapofafanua kuwa sitiari nyingi zinazotumiwa katika mziki huu zinasawiri tabia zisizofaa za mwanamke. Kwani anaonekana kuwa kiumbe asiye na msimamo kwa kutumiwa na wanaume kama chombo cha kujistarehesha.

Hata hivyo, tukichunguza kwa makini tutaweza kubaini kuwa, matokeo hayo yanasababishwa na hali za kimaisha za mwanamke. Ni tabia ambazo zinafanywa na wanawake kutokana na kugubikwa na hali ya utegemezi na hasa utegemezi wa kiuchumi. Kwani katika muktadha ambao mwanamke si tegemezi tena wa mwanaume, anaelezwa katika bongo fleva, kuwa mtu mwenye msimamo na asiyekubali kudanganywa na wanaume au hata kutumiwa na wanaume kama chombo cha starehe. Katika wimbo wa *Mademu Watafutaje* baadhi ya mistari ifuatayo inadhihirisha jambo hili

> "Ana msimamo kama Magreth J,...
>
> hajajitumbukiza kwenye umalaya...........
>
> Hana mapepe......................." .

Hivyo, matokeo yanayoelezwa na Mnenuka (2010) na Jilala (2010) huenda yanatokana na hali za kiuchumi, pengine wanawake wanaotumiwa na wanaume kama chombo cha starehe hufanya hivyo ili wapate fedha za kujikimu kimaisha.

Hivyo, kukosa msimamo katika maisha si tu hufanywa na wanawake kwa sababu ya jinsi zao, la hasha! Hutokea kutokana na utegemezi wa kimaisha. Ni jambo ambalo linaweza kufanywa na wanaume pia katika muktadha ambao mwanamume ni masikini na tegemezi kwa mwanamke kama ambavyo inajitokeza pia katika nyimbo za bongo fleva. Kwa mfano, katika wimbo wa Lady Jay dee *Wanaume kama Mabinti* msanii anawakebehi wanaume ambao huwategemea wanawake kimaisha, kwa kuwafananisha na wanawake wanaouza miili yao. Tunachoweza kusema hapa ni kwamba, hali ngumu ya kimaisha ndiyo chanzo cha wanawake kukosa msimamo ndani ya jamii. Aidha, wanawake ambao si tegemezi wanatajwa katika muziki wa bongo fleva kuwa wenye msimamo na wenye bidii ya kufanya kazi.

**Ni Mwezeshaji na Mwanaharakati wa Maendeleo ya Jamii**

Pamoja na kwamba tahakiki nyingi zinamtaja mwanamke kama kiumbe tegemezi kwa mwanamume, mwanamke naye anaweza kuwa msaada kwa jamii yake kimaendeleo pale anapokuwa na uwezo wa kiuchumi. Kwa mfano katika *Zali la Mentali*, mwanamume anafurahia anapokutana na mwanamke wa aina hii: Anasema ni **Zali** akiwa na maana kuwa amepata bahati asiyotarajia. Katika wimbo huu tunaelezwa kuwa hali ya unyonge na umasikini wa mwanamume inatoweka baada ya kuwezeshwa na mkewe, maisha yake yanabadilika na kuwa yenye raha na furaha. Kwa hiyo, mwanamke hapa anaonekana kuwa anaweza kuleta maendeleo kwa familia na hata kwa jamii yake.

Aidha, ingawa katika wimbo wa *Wanaume kama Mabinti* msanii anawakejeli wanaume wanaopokea vitu kutoka kwa wanawake hata hivyo, wimbo huu unatuonesha kuwa mwanamume anaweza kupata maendeleo kutoka kwa mwanamke tofauti na ilivyozoeleka kuwa wanawake ndiyo tu huwezeshwa na wanaume. Katika wimbo huu wanawake wanatajwa kuwa ni wanaharakat wa maendeleo. Neno watafutaji linasadifu vyema hili, kwani linarejelea watu wanaojituma wenye kufanya kazi kwa bidii (bila kuchoka). Hivyo, mwanamke anaonekana kuwa mpenda maendeleo.

**Uhusiano na Jamii**

Katika makala haya swali mojawapo lililokuwa linaulizwa ni je, wanawake huwa wamekidhi matarajio ya jamii? Uhusiano wao na jamii kwa ujumla ukoje? Uhusiano huu ni muhimu kuutazama kwani kama wanawake ambao tayari wameshapata fursa hawaonekani kukidhi yale ambayo jamii iliyatarajia, basi hii inaweza kuwa sababu inayokwamisha mwendelezo wa jitihada za kuwakwamua wanawake. Katika wimbo wa *Machozi Jasho na Damu* wa Prof J msanii anasema:

> "Mkutano wa Beijing ungefanyika kijijini, labda na bibi yangu angekuwepo Kundini"

Kauli hii ni kama inawashutumu wanawake ambao tayari wameshafanikiwa ambao hata hivyo wamesahau kuwakomboa wengine. Mkutano wa Beinjing unaotajwa uliwakutanisha wanawake ambao wana nafasi duniani na fursa za juu za maendeleo. Hata hivyo, msanii anaona kuwa mkutano huu ungekuwa na tija zaidi kama ungeshirikisha wanawake kutoka vijijini na sehemu ambazo bado zipo nyuma kimaendeleo. Hivyo, anaona mkutano kama huu ulipaswa kufanyika mahali ambapo kuna kundi/idadi kubwa ya wanawake ambao bado wamefungwa katika minyororo ya unyonge na utegemezi. Pengine hapa msanii anatoa rai kuwa, ukombozi wa dhati hauwezi kupatikana kama mikakati itabagua kundi kubwa la wanawake hasa wale wa vijijini.

Vilevile, katika nyimbo za *Zali la Mentali* na *Mtoto wa Geti Kali*, hali ya utabaka inaonekana dhahiri. Kwamba wanawake wakiwa katika hali fulani (ya juu) ya kimaisha huwabagua watu wengine na hasa wanaume. Ingawa wanawake hufanya hivyo, kwa upande wao wanaume wenye uwezo hawafanyi hivyo na badala yake wanawake huwakimbilia ili kuondokana na ugumu wa maisha.

Pengine hali hii inaleta hofu kwa jamii, kuhusiana na uwezeshaji wa wanawake, kwamba endapo wanawake wote watakuwa na nguvu na mamlaka ndani ya jamii huenda utabaka unaweza kushamiri sana. Hivyo, kutokana na utabaka unaolalamikiwa katika *Mtoto wa Geti Kali* na *Zali la Mentali*, tunaweza kusema kuwa jamii inawatuhumu wanawake, wenye mafanikio kwa kujitenga na kundi kubwa la wanajamii, kutokana na kushindwa kuwashirikisha wale ambao bado wako nyuma.

Uchambuzi huu (hapo juu) umetumia nyimbo za bongo fleva zilizoimbwa na wasanii wa kiume kwa kiasi kikubwa. Maelezo yanayofuata yanachambua usawiri wa mwanamke katika nyimbo zilizoimbwa na wasanii wa kike.

**Mtazamo wa Wasanii wa Kike**

Katika nyimbo zilizoimbwa na wasanii wa kike ni ajabu kuwa wao wenyewe hawakubaliani na uhuru wao. Ingawa hakuna nyimbo nyingi zinazozungumzia jambo hii hata hivyo wimbo wa Lady Jaydee *Wanaume kama Mabinti* ni mfano mzuri.

Katika wimbo huu msanii anawakejeli na kuwakebehi baadhi ya wanaume wanaobweteka na mali wanazopata kutoka kwa wapenzi/wake zao. Msanii anatumia lugha kali kwa kuwafananisha na machangudoa. (wanawake wanaouza miili yao). Kwa mfano anasema:

> "Utawaona kwenye magari ya mademu zao,
> Wakitanua na kucheka utadhani yao.........."

Ingawa nia ya wimbo huu ni kuwakejeli wanaume wasiotia bidii katika kufanya kazi na kujipatia mali zao wenyewe, hata hivyo tunaweza kuona mtazamo wa msanii huyu unawakilisha mawazo ya wanawake wenyewe kushindwa kujikubali kuwa wanaweza kutoa msaada kwa jamii inayowazunguka hasa waume au wapenzi wao. Kupitia wimbo huu, inaonekana msanii anaamini kuwa suala la kumiliki mali kama vile majumba, magari n.k. na kisha kutumia mali hizi na mwenza ni suala ambalo linapaswa kufanywa na wanaume na sio wanawake. Kwa maana nyingine ni kuwa mwanamume akimtegemea mwanamke hadhi yake inashuka, (ndiyo maana yeye anawafananisha na wanawake wanaouza miili yao) kwa hakika hizi ni fikra duni ambazo zinazidi kuendeleza mawazo kuwa mwanamke au binti ni kiumbe tegemezi, na anayehitaji kufadhiliwa na mwanaume. Kuendelea kusema kuwa wanaume tegemezi ni sawa na mabinti ni sawa na kujidhalilisha wenyewe.

**Hitimisho**

Pamoja na kuwa mwanamke anachukuliwa kuwa kiumbe dhaifu, duni, tegemezi na asiye na msimamo, (Mnenuka, 2010; Omari, 2006 na Jilala, 2010) hata hivyo, hali hii haitokani tu na mfumo dume na utamaduni kandamizi unaomzunguka mwanamke, bali pia umasikini wa kipato na kifikra huenda ni sababu kuu. Vilevile, inawezekana kinachowainua wanaume katika jamii na kuwa wenye uwezo na mamlaka ni nguvu za kiuchumi hususan fedha na elimu ingawa kama aelezavyo Schipper (2006) utamaduni wa jamii nao unampa fursa zaidi mwanamume. Kupitia nyimbo hizi za bongo fleva kama *Narudi Kijijini* tunaona kuwa katika muktadha ambao mwanamume hana fedha maisha yake ni duni, ni mnyonge kama wanawake wengi wanavyosawiri katika kazi za fasihi nyingi naye anaweza kutumiwa na mwanamke kama chombo cha starehe. Mwanamke mwenye pesa anaweza kunyanyasa, kudhalilisha kumnunua mwanamume na kumtumia kwa matakwa yake. Kuna haja ya kufanyika

utafiti zaidi kuhusiana na usawiri wa mwanamke katika bongo fleva na fasihi kwa ujumla. Inaonekana mahitimisho mengi yanayotolewa na wahakiki huenda yanaegemea zaidi katika sura moja ya mwanamke tegemezi na mnyonge hivyo utafiti zaidi unahitajika katika tanzu nyinginezo za fasihi kwa kuangalia sura nyingine ya mwanamke ambaye ameshajikomboa katika masuala ya kiuchumi na hata kielimu. Vilevile, kutokana na matokeo yaliyoelezwa katika makala haya, kuna haja pia ya kuchunguza zaidi kuhusiana na jinsia za watunzi wa nyimbo hizi. Kwani kwa kawaida muimbaji si lazima akawa mtunzi wa wimbo husika.

**Marejeleo**

Jilala, H. (2010). 'Lugha na Jinsia katika Ushairi. Uchunguzi wa Sitiari za UKIMWI na Mapenzi katika Mashairi ya Bongo Fleva' katika *Mulika* Na. 29 &30. Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya. Taasisi ya Taaluma za Kiiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Matteru M. L. B (1982). 'The Image of the Woman in Tanzania Oral Literature: A Survey' katika Jarida la *Kiswahili* Juzuu ya 49/2 la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Mnenuka, A. (2010). 'Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule' katika *Mulika* Na. 29&30. Toleo Maalum la Muziki wa Kizazi Kipya. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Momanyi, Clara (2001). 'Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert' katika Jarida la *Kiswahili* Juzuu Na. 64 la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omari, S. (2006). 'Mitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania' katika Jarida la *Kiswahili* Juzuu Na. 69 la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omari, S. (2008). 'Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania' katika Jarida la *Kiswahili* Juzuu Na. 71 la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Schipper, M. (2006). *Never Marry a Woman with Big Feet: Women In Provebs from Around the World*. Amsterdam: Amsterdam University Press.

Swaleh, A. (1997). 'The Image of Woman in S. A. Mohamed's Tata za Asumin' katika jarida la *Kiswahili* Juzuu Na. 60 la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.